



# Uamuzi

 Ursula Nafula

 Vusi Malindi

 Ursula Nafula

 2

 Kiswahili SW



Kijiji changu kilikuwa na matatizo mengi.  
Tulipanga foleni ndefu tukisubiri kuchota maji  
kutoka mfereji mmoja.




Tulisubiri kupokea msaada wa chakula.



Tulifunga nyumba zetu mapema kwasababu ya wizi.



Watoto wengi waliacha shule.



Wasichana wadogo walifanya kazi za nyumbani kwenye vijiji vingine.



Wavulana wadogo waliranda randa kijijini na wengine walifanya kazi kwenye mashamba ya watu.



Upepo ulipovuma, ulipeperusha karatasi chafu na kuzifikisha mitini na uani.





Watu walikatwa na vipande vya chupa vilivyotupwa ovyo ovyo.



Halafu siku moja, mfereji wa maji ulikauka na mitungi yetu ikawa mitupu.



Baba yangu alitembea nyumba hadi nyumba akiwaomba watu kuhudhuria mkutano wa kijiji.



Watu walikusanyika chini ya mti mkubwa na kusikiliza.



Baba yangu alisimama na kusema, “Tunahitaji kusaidiana kutatua matatizo yetu.”



Juma, mtoto wa miaka minane aliyekuwa amekaa kwenye tawi la mti, alisema kwa sauti, "Naweza kusaidia na usafi."



Mwanamke mmoja alisema, “Sisi wanawake tunaweza kuungana na kulima.”



Mwanamume mwingine alisimama na kusema, “Wanaume watachimba kisima cha maji.”





Sote tulisema kwa sauti moja, “Lazima tubadilishe maisha yetu.” Tangu siku hiyo, tulifanya kazi pamoja kutatua shida zetu.



# Global Storybooks

[globalstorybooks.net](http://globalstorybooks.net)

## Uamuzi

 Ursula Nafula

 Vusi Malindi

 Ursula Nafula

